SOMO LA NANE: MAFUNZO YA BIBLIA KUHUSIANA NA KIFO

"Kwa maana walio hai wanajua kwamba watakufa; lakini wafu, hawajui lolote kamwe, wala hawana malipo tena, kwa maana kumbukumbu lao limesahauliwa. Pia, upendo wao na chuki yao na wivu wao tayari zimepotea, na mpaka wakati usio na kipimo hawana fungu lolote tena katika chochote ambacho kitafanywa chini ya jua." (Mhubiri 9:5-6)

Mafundisho ya Maandiko juu ya hali ya kifo yako wazi na yanapatana kabisa na suala la somo la awali kuhusu hali ya kufa na udhaifu wa wanadamu. Hapa tena tunapaswa kuelewa mafundisho ya Biblia nkwa kuelewa kanuni na umuhimu wa mpango wa Mungu wa wokovu.

Kwa bahati mbaya, mafundisho ya Biblia yanaendelea kuwa tofauti na mafundsisho ya makanisa ya kawaida juu ya hili somo muhimu. Ni bahati mbaya kwa sababu bila kuelewa sahihi kwa nini Biblia inafundisha kuhusu kifo, haiwezekani kufahamu upendo wa Mungu wa kuanzisha njia ya ukombozi kutoka kwa kifo *kwa njia ya Ufufuo* hadi maisha mapya. Kwa kweli, wazo maarufu na la jadi ya kuelekea moja kwa moja hadi mbinguni au kuzimu baada ya kifo, kama malipo au adhabu, *inaondoa haja ya ufufuo kabisa ,* na inaondoa maana yoyote ya maandiko ya Biblia kuhusu swala hili muhimu.

"Kifo" kimepoteza maana yake yote ikiwa wafu hawajafa, lakini"wamekwenda mbele" na "kumsifu Mungu sasa mbinguni." Hakuna ushahidi wa maandiko kwamba wafu wamekwenda popote, au hata kuwa wako katika hali fulani ya ufahamu. Lakini kuna ushahidi mwingi wa kuonyesha kuwa wamekwenda kaburini, na hawajui kabisa, na wamekuwa kama ambao hawakuwepo kamwe. Kwa mfano-

"Mtu wa udongo, ingawa katika heshima, ambaye haelewi, Kwa kweli analingana na wanyama ambao wameangamizwa." (Zaburi 49:12, 20)

Kifo ni kinyume cha maisha. Tunajua maisha ni nini kwa mujibu wa uzoefu. "Kifo" ni neno ambalo linamaanisha kukatiza maisha au mwisho wa maisha. Maisha yameonyeshwa na shughuli ya kupumua, mzunguko wa damu, na kuponda chakula. Moyo, mapafu na tumbo hutupa shughuli inayoitwa "uzima" katika miili yetu. Bila viungo hivi, maisha haya hayapo. Tukishtua ubongo wetu, tunapoteza busara, na ikiwa tunazuia hewa yetu, tunashindwa kupumua. Tukiwaacha ugavi wetu wa chakula, njaa ifuatavyo, na maisha huisha. Utaratibu huu unathibitishakuwa maisha yanategemea mpangilio wa utaratibu wa kazi za miili yetu

Tunapozungumza kuhusu wanyama, hii ndio jinsi tunavyotumia maneno haya "maisha" na "kifo". Tukirejelea wanyama hatuna ugumu na maana ya wazi ya maneno haya. Maandiko yanasema kuwa kwa maumbile ya kimwili, binadamu na wanyama ni sawa: Wote ni "nafsi hai", "viumbe hai".

Tunapasa kutambua kwamba kulikuwa na wakati uliopita wakati kila mmoja wetu hakuwepo kabisa, wakati miili yetu haikuwa ilivyo. Kwa hiyo ina maana kwamba uharibifu wa miili yetu itasababisha tusiwepo kabisa.

"Kwa maana wewe ni mavumbi nawe utarudi mavumbini." (Mwanzo 3:19)

Kifo huja kubatilisha kile kilichoanza wakati wa kuzaliwa. Kuzaliwa husababisha uwepo, bali kifo huundoa kabisa. Ni wazi kuuona uhusiano huu katika wanyama. Sisi na wao ni sawa tu.

Wakati Biblia inapozungumzia kifo cha watu wowote wa Mungu, haisemi kuwa “wameenda kupata zawadi” au “wameelekea katika njia ya utukufu”, au wazo lolote kama hilo. Kwa mfano, inaonyesha kumbukumbu ya vifo vya baba watakatifu wa kabila la Wahayudi kwa njia hii iliyo wazi –

Ibrahimu: (Mwanzo 25:8)

“Alifariki baada ya kuishi maisha marefu na ya fanaka, akajiunga na wazee wake waliomtangulia.”

Isaka: (Mwanzo 35:29)

“Kisha Isaka akakata pumzi, akafa, naye akakusanywa kwa watu wake, akiwa mzee na mwenye kutosheka na siku, na Esau na Yakobo wanawe wakamzika.”

Yakobo: (Mwanzo 49:33)

“Yakobo alipomaliza kuwausia wanawe, aliirudisha miguu yake kitandani, akatoa roho akajiunga na wazee wake.”

Yusufu (Mwanzo 50:26)

“Basi, Yosefu akafariki kule Misri, akiwa na umri wa miaka 110. Nao wakaupaka mwili wake dawa usioze, wakauweka katika jeneza kule Misri.”

Musa (Kumbukumbu la Torati 34:5)

“Kisha Musa mtumishi wa Yehova akafa huko katika nchi ya Moabu kama Yehova alivyosema.”
Kati ya wale wote amabo mauti yao imeandikwa katika maandiko, haisemekani kuwa wamekweenda popote; ila wanazungumzia kuwa *wanakufa, wanaacha maisha yao, na kurudi chini*, kama vile Mungu alivyomwambia Adamu. Angalia nini kinachosemwa juu ya waumini wa Paulo:

“Watu wote hawa walikuwa bado wanaishi kwa imani walipo kufa. Hawakupata yale waliyoahidiwa; lakini waliyaona na kuyafurahia kwa mbali.” (Waebrania 11:13)

Wakati Yesu alizungumza juu ya kifo cha Lazaro, alikuwa sawa kabisa-

“Lazaro rafiki yetu anapumzika, lakini ninafunga safari kwenda huko ili kumwamsha kutoka usingizini. Kwa hiyo wanafunzi wakamwambia: “Bwana, ikiwa anapumzika, atapona. Kwa hiyo, wakati huo, Yesu akawaambia waziwazi: “Lazaro amekufa,” (Yohana 11:14)

<PG 3>

Je! Yesu angewezaje kusema Lazaro *amelala*,na anahitaji *kuamshwa* , ikiwa wakati huu wote alikuwa macho mbinguni, akimsifu Mungu?

Kwa Stefano, Biblia inasema vile vile, alipokufa –

“Alilala” (Matendo ya Mitume 7:60)

Na Paulo alipowaandikia Wathesolanike juu ya wenye haki waliokufa, kuwafariji (hakika huu ulikuwa wakati mzuri wa kuwaambia kuwa walikuwa hai na wenye furaha mbinguni!), yeye alielezea kifo chao kama *usingizi,* na kwamba watafufuliwa kutoka kwa wafu wakati wa kurudi kwa Kristo. (1 Wathesolanike 4:13-18)

“Zaidi ya hayo, akina ndugu, hatutaki mkose kujua kuhusu wale walalao usingizi katika kifo; ili msiwe na huzuni kama wale watu wengine wasio na tumaini. Wale ambao wamelala usingizi katika kifo kupitia Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye.”

Hakunavizuizi kwa mifano hii kutoka kwa kumbukumbu za Biblia. Biblia daima inazungumzia kifo kama mwisho wa maisha, na sio kama mwanzo wa hali nyingine. Wafu daima huwakilishwa kama wasio na fahamu, wasiojua chochote (isipokuwa katika sehemu mbili: ya kwanza kwa mfano wa kishairi- Isaya 14:14; nyingine kwa hadithi kutumia ushirikina wa Mafarisayo kufundisha somo muhimu – Luka 16:19-31). Maelezo halisi ya Maandiko yako wazi kuwa, wafu daima huzungumziwa kuwa ni “Nchi ya usahaulifu”, “nchi ya giza”. “kimya”,”uharibifu”, na “kutojua”.

Sulemani akasema –

“Yote ambayo mkono wako unapata kufanya, yafanye kwa nguvu zako zote, kwa maana hakuna kazi, wala utungaji wala ujuzi wala hekima katika Kaburi, mahali unapokwenda.” (Mhubiri 9:10)

Ayubu, aliyekuwa mgonjwa, kwa dhiki yake ya majaribio, alisema haya kuhusu kaburi (Ayubu 3:13-19)

“ Humo waovu wameacha msukosuko, Na humo wale walioishiwa nguvu wanapumzika. Wafungwa wamestarehe pamoja;Kwa kweli hawaisikii sauti ya mtu anayewalazimisha kufanya kazi. Wadogo na wakubwa wamo mle pamoja, Naye mtumwa anawekwa huru kutoka kwa bwana wake.”

Alisema kuwa alitamani kufa akiwa angali mtoto. Alisema kwamba angeweza *“kulala tuli na kuwa na utulivu”*. **Hakuna kurejelea kuwa mbinguni** kama inavyofundishwa. He said he should have –

“Ningalilala wakati huo; ningalikuwa ninapumzika pamoja na wafalme na washauri wa dunia, singalikuwako, kama watoto ambao hawajaona nuru.”

Aliongeza zaidi, baadae katika kesi yake –

*“Basi kwa nini ulinitoa nje ya tumbo la uzazi? Kama ningekata pumzi (**gava** ;iliyopumuliwa), ili hata jicho lisinione Ningekuwa kana kwamba sijapata kuwako” (Ayubu 10:18)*

Mwandishi wa Zaburi Daudi alikuwa wazi vile vile (Zaburi 88:10-12)

"Je, wale wasiojiweza katika kifo watasimama. Je, watakusifu wewe? Sela*. Je, fadhili zako zenye upendo zitatangazwa katika kaburi,Na uaminifu wako katika mahali pa maangamizi? Je, jambo lako la ajabu litajulikana katika giza, Au uadilifu wako katika nchi ya usahaulifu?"*

Jibu hasi linatolewa na kalamu iyo hiyo iliyofunuliwa (Zaburi 115:17)-

"Wafu wenyewe hawamsifu Yah, wala wowote wanaoingia mahali penye kimya"

Alisema kuwa *uhai* ni wakati wa kumtumikia Bwana, kufanya mapenzi yake kwa kujifunza Neno Lake na kuimba nyimbo zake za sifa:

"Nitamsifu Yehova muda wote wa maisha yangu. Nitampigia Mungu wangu muziki maadamu nipo."(Zaburi 146:2)

Ni wazi kwa dhana ya Daudi kuwa uhai wake ungeisha na tuko la kifo. Zingatia yale Sulemani na hekima ya Uungu alitangaza (Mhubiri 9:5-6)

"Kwa maana walio hai wanajua kwamba watakufa; lakini wafu, hawajui lolote kamwe, wala hawana malipo tena, kwa maana kumbukumbu lao limesahauliwa. ***Pia, upendo wao na chuki yao na wivu wao (yaani uwezo wa mawazo)tayari zimepotea****, na mpaka wakati usio na kipimo hawana fungu lolote tena katika chochote ambacho kitafanywa chini ya jua."*

Hii ilikuwa imesisitizwa awali na baba yake Daudi.

"Msiweke tegemeo lenu katika watu wenye vyeo, Wala katika mtu wa udongo, ambaye hana wokovu wowote. Roho yake hutoka, naye hurudi kwenye udongo wake; Siku hiyo mawazo yake hupotea."

"Kwa maana katika kifo wewe hutajwi,Katika Kaburi ni nani atakayekusifu?"

Hii inatuwacha bila shaka kuhusu hali ya wafu. Lengo la nafsi isiyoweza kufa ni kuwepo na Mungu; bali hii inasema kwamba **baada ya kifo hakuna kumbukumbu ya Mungu.**
Hezekia, mfalme mwenye haki wa Yua, aliyekuwa mgonjwa "karibu kufa" alikuwa amepona, alimsifu Mungu kwa njia ifuatayo –

" Kwa maana Kaburi haliwezi kukusifu; kifo hakiwezi kukusifu. Wale wanaoshuka shimoni hawawezi kuutumaini ukweli wako. Aliye hai, aliye hai, ndiye anayeweza kukusifu, Kama vile mimi ninavyoweza leo hii.." (Isaya 36:18-19)

Biblia inafundisha kwamba kifo ni kupoteza kabisa hali ya kuwepo, fahamu zetu kusimama kabisa, usingizi wa ndoto katika "vvumbi ya dunia"

Mambo haya huanzisha umuhimu kabisa wa ufufuo, kwa sababu ya maandiko yaliyotangulia, hitimisho nzuri amabyo tunaweza kufikia ni kwamba maisha ya baadaye yanapatikana tu kwa ***ufufuo kutoka kwa wafu.*** Katika kila mfano, imani maarufu kuhusu wafu ni kinyume hasa na taarifa wazi ya Biblia. Hakuna

ahadi hata moja ya kwenda mbinguni wakati wa kufa katika Biblia nzima; Hamna alama hata moja kuonyesha kuwa binadamu ana “nafsi isiyoweza kufa”, au kitu kingine chochote kinachoishi baada ya kifo. Ukweli wa msingi uliosisitizwa mara kwa mara ni:

“WAFU HAWAJUI CHOCHOTE”

Somo la kufuata: MAFUNDISHO YA BIBLIA KUHUSU MBINGU NA JAHANAMU

Jina Bw/Bi ……
Anwani …….. Msimbo la posta …….

*Unaweza kuhitaji karatasi ya ziada kwa majibu yako iwapo hakuna nafasi ya kutosha hapo chini. Hii itakusaidia wewe – na sisi – kujua kiasi gani ulichogundua kuhusu Biblia yako. Tafadhali rudisha fomu hii kwenye bahasha zilizotolewa hata kama huwezi kujibu maswali yote. Tunapopokea tutaendelea kujifunza zaidi.

MASWALI KUHUSU SOMO HILI

1. Wazo la kuelekea mbinguni au jahanamu moja kwa moja baada ya kifo lina athari gani juu ya mafundisho ya ufufuo.
2. Nini maana ya “maisha”?
3. Tunaelewa nini kuhusu maana ya kifo?
4. Ni nini kinachoanza wakkati wetu wa kuzaliwa ambacho hukamilika wakati wa kifo chetu?
5. Je, Biblia inafundisha kuwa tunapata thawabu wakati wa kifo chetu?
6. Biblia inasema ni nini kilichotokea Abrahamu, Isaka na Yakobo walipokufa?
7. Biblia inaelezea kifo cha mtu yeyote Yule vipi?
8. Waebrania 11 inaelezea nini kuhusu waaminifu na malipo yao?
9. Yesu alielezea kifo cha Lazaro wa Bethnia katika njia zipi mbili?
10. Kifo cha Stefano kilielezwaje katika Matendo ya Mitume 7:60?
11. Biblia inazungumzia wafu kuwa katika maeneo au hali gani?